**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Public Private Partnership | Public Private Partnership (PPP) Documents

2020

# Mradi wa Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Tanzania,2020

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara Ya Fedha na Mipango

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/397

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*


# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

**MRADI WA UBIA KATI YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI TANZANIA (P159192)**

**KUTANGAZWA KWA UTARATIBU WA KUSIMAMIA MAZINGIRA NA JAMII (ESMF)**

**Desemba, 2020**



## 1. UTANGULIZI

Serikali ya Tanzania (GoT) inatekeleza Miradi Ushirikiano wa Umma na Binafsi (PPPs) ili kujenga miundombinu na kuimarisha huduma za umma. Utekelezaji unaongozwa na Sera ya Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP) iliyoidhinishwa mwaka 2009, Sheria ya PPP Sura ya 103 na Kanuni za PPP za 2020.

Mradi unaopendekezwa wa wa Mradi wa Ushirikiano wa Umma na Sekta Binafsi (TPPP) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) ni dola milioni 14 na utasaidia Wizara, Idara na Wakala wa Serikali (MDAs) na mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) kutekeleza Programu ya PPP. TPPP itasaidia Kituo cha PPP kilichopo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP), Kitengo cha PPP (*PPP Node)* kilichopo Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Mamlaka za Serikali (CA) zinazotekeleza miradi. TPPP itazingatia yafuatayo:

a) Uandaaji na ununuzi wa miradi ya PPP,
b) Kuimarisha misingi ya PPPs (kujenga uwezo), na
c) Ufuatiliaji na Tathmini.

Miradi ya PPP inayostahiki msaada wa TPPP itajumuisha (i) miradi mikubwa, kama vile ya miundombinu ya usafirishaji, uzalishaji wa umeme, usambazaji wa maji, afya, elimu, na habari, mawasiliano na teknolojia, na (ii) miradi midogo midogo, kama vile masoko ya kisasa , vituo vya basi na daladala, usimamizi wa takangumu na maji, na hosteli za wanafunzi. Miradi mingine itaboreshwa na mininge itakuwa mipya kabisa. Kazi za TPPP zitangingatia mahitaji lakini hazitakwenda Zaidi ya wigo wa madhara ya kama itakavyoinishwa.

## 2. ATHARI ZA MAZINGIRA NA JAMII

Utekelezaji wa TPPP utasababisha athari chanya na hasi kupitia mradi mmoja mmoja wa PPP ambao unasimamiwa na TPPP. Athari nyingi zitatokana na shughuli za ujenzi wa miradi ya PPP, na nyingine zitatokea wakati wa utekelezaji wa miradi. Athari zinazoweza kujitokeza ni pamoja na:

### *2.1 Athari chanya ni Pamoja na:*

- Kuongezeka kwa ubora wa huduma na majengo;
- Kuongeza ufanisi;
- Kupunguza msongamano;
- Kuboresha usalama ulioboresha wa wateja, wafanyabiashara na watoa huduma;
- Majengo bora ya kutolea huduma;
- Fursa za ajira na za biashara kwa jamii wakati wa ujenzi na uendeshaji wa mradi;
- Kuongezeka kwa thamani ya ardhi katika maeneo ya karibu na mradi;
- Kuboreshwa kwa maisha ya waendeshaji, wafanyabiashara, wachuuzi na watoa huduma; na
- Kuboreshwa kwa usafi wa mazingira na kupunguza hatari za kiafya.

## *2.2 Athari hasi ni Pamoja na:*

i. Kero ya kelele zitokanazo na mitambo ya ujenzi, kuongezeka kwa magari barabarani na shughuli nyingine za kiuchumi;
ii. Uchafuzi wa udongo au maji kutokana na kuzagaa kwa maji taka yanayotoka kwenye mabomba ya majitaka yasiyofanya kazi vizuri au kutokuwepo na mifumo ya kutibu maji-taka na taka na kuwa maji yanayovujia kwa juu kutokana shughuli za ujenzi na uendeshaji wa mradi;
iii. Kuathiri vyanzo vya maji ardhini na kuwa na ukosefu wa maji ardhini kutokana na matumizi makubwa ya maji kutoka kwenye miamba ya maji.
iv. Uharibifu wa ardhi kwa njia ya mmomonyoko, mgandamizo, kuziba na /au kujaa maji) kutokana na shughuli za ujenzi (kusawazisha barabara, kuondoa uoto na kuwa na mashimo ya kuchimba udongo);
v. Ongezeko la uchafu unatoka kwenye mashimo makubwa ya kuchimba mchanga na kokoto kwa ajili ya ujenzi na hivyo kusababisha kutuama kwa maji yenye kemikali (mabwawa yenye asidi), endapo mashimo hayo hayatafukiwa;
vi. Uchafuzi wa hewa unaotokana na uendeshaji wa mitambo ya ujenzi na majenereta;
vii. Kuongeza kwa hatari za kiafya, kiulinzi na kiusalama kwa umma na kwa wajenzi;
viii. Kuongeza hatari ya ajali za moto unaoweza kuharibu mali na na maisha ya wakazi;
ix. Kupoteza majengo au mazao;
x. Kupoteza kipato au biashara;
xi. Kupotea kwa maeneo ya wazi au kuongezeka kwa maeneo yaliyozuiwa watu kuingia;
xii. Kupoteza kipato kwa muda kwa sababu ya kuhamishwa kwenye majengo, na pengine kupoteza kipato moja kwa moja endapo haki za kurejea kwenye majengo hayo hazitatolewa;
xiii. Kuwatenga wazawa katika zabuni za ujenzi, uendeshaji pamoja na ajira;
xiv. Kuharibu maeneo ya kihistoria au ya kiutamaduni, au rasilimali za kitamaduni; na
xv. Kuvuruga mfumo wa maisha wa wenyeji ambao walizoea kuwa nao.

# 3 MALENGO

i. TPPP inahimiza matumizi ya Sera ya Tathmini ya mazingira ya Benki ya Dunia (OP / BP 4.01). Miradi yote ya PPP inayosimamiwa na TPPP itafanyiwa tathimini kuangalia kama kuna athari za mazingira na jamii na ndipo baadaye tathmini ya athari za mazingira na jamii itafanyika. TPPP itasaidia miradi ya PPP iliyo kwenye kundi B au C pekee kwa mujibu wa Sera za Benki ya Dunia.

ii. Miradi ya PPP iliyo kwenye maeneo nyeti ya kiikolojia kama vile maeneo tengefu au ya hifadhi za mazingira na ya Kundi A kama yalivyofafanuliwa kwenye OP/BP 4.01 haitakuwa na sifa ya kusaidiwa. Miradi ya PPP inayohitaji upatikanaji wa ardhi kwanza kabla ya kuanza kutekelezwa nayo itaondolewa kwenye usimamizi wa TPPP. Shughuli za TPPP zitafanyika tu katika miji mikubwa na maeneo yaliyo nje kidogo ya miji na haitasaidia miradi iliyo katika maeneo ya vijijini ambako kuna makundi ya watu wasiojiweza.

iii. Mfumo huu wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii (ESMF) ulitayarishwa kwa ajili ya kuweka taratibu, mawanda na mahitaji kwa lengo la: kufanya uchunguzi wa hali ya Mazingira na Jamii; kukamilisha Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii (TAM); kueleza kuhusu mchakato wa uhakiki; na, kutoa idhini na hatua za utekelezaji wa miradi ya PPP ambayo itasimamiwa na TPPP. ESMF pia inaelezea dhima na majukumu na namna ya kujenga uwezo kwa ajili ya kuhakikisha kuwa kunakuwepo na ufanisi katika utekelezaji wa miradi.

iv. Athari za kuhamisha watu kwenye makazi yao pasipo hiyari yao zitashughulikiwa katika Mfumo tofauti wa Sera ya Uhamishaji wa Makazi (RPF). RPF inahusu maandalizi na utekelezaji wa Mipango ya Uhamishaji wa Makazi (RAP) na Mipango Iliyofupishwa ya Hatua za Uhamishaji wa Makazi (ARAP).[1]

## 4 MCHAKATO WA TATHMINI YA MAZINGIRA NA JAMII

TPPP itasaidia tu mchakato wa kumpata mbia kutoka sekta binafsi kwa ajili ya mradi wa PPP baada ya Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii (TAM) kuandaliwa na Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kutoa cheti cha Tathmini ya Athari za Kimazingira kwa mradi wa PPP. TAM lazima ikidhi matakwa ya Kanuni za Ukaguzi wa Athari za Mazingira za mwaka 2005, 2018 na sera na miongozo ya usalama wa miradi ya Benki ya Dunia. TPPP inatarajiwa kufadhili maandalizi ya TAM na kupata cheti cha TAM. TPPP pia inaweza kusaidia miradi ya PPP ambayo imefanya TAM na kupata Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii (TAM).

Sifa za mchakato wa tathmini ya Mazingira na Jamii ni:

i. **Uchunguzi wa Awali**: Kabla ya kuanza mchakato wa kumpata mbia kutoka sekta binafsi kwa ajili ya mradi wa PPP, mradi huo wa PPP utachunguzwa mara moja tu kwa ajili ya: 1) kuangalia kama mradi huo wa PPP una sifa za kusimamiwa na TPPP; 2) kugawanya makundi ya viatarishi kwa mujibu wa Kanuni za Ukaguzi wa Tathmini ya Athari za Mazingira (2005) kama zilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2018 na Sera ya Tathmini ya Mazingira ya Benki ya Dunia (OP / BP 4.01) kwa lengo la kuamua mawanda na mahitaji ya kina ya TAM, wakati bado hayajatayarishwa; 3) kubainisha sera za usalama wa miradi za Benki ya Dunia zinazofaa kutumika pamoja na mahitaji mengine; na 4) kubainisha masuala mahusus ambayo vitengo vya PPP na Mamlaka za Usimamizi wa Miradi vitahitaji msaada wa kitaalamu.

   Fomu ya Uchunguzi wa Mazingira na Jamii itakamilishwa kwa miradi yote ya PPP itakayosimamiwa na TPPP. Taarifa zilizomo kwenye fomu hii zitaelezea aina, eneo, unyeti wake, ukubwa wa mradi na kiwango cha ukubwa wa athari za mazingira na kijamii zinazoweza kujitokeza. Fomu hii itakuwa msingi wa kuamua kundi la mradi kwa kulingana na mwongozo uliotolewa na OP/BP 4.01. Ikiwa mradi utaangukia Kundi A, basi mradi huo utawekwa kando maana hautastahili

[1] Sera ya Usalama wa Miradi ya Benki ya Dunia OP 4.12 – kuhusu kuhama makazi kwa lazima inaeleza kuwa, "endapo hakutakuwa na madhara makubwa ya mradi kwa watu wengi, au watakaohamishwa ni chini ya watu 200 , basi Mpango Mdogo wa Kuhamisha Makazi unaweza kukubalika kutumika…Madhara yanayotambulika kuwa ni madogo endapo wale watakaoathirika na mradi hawajahamishwa ni wanapoteza chini ya asilimia 10 ya mali zao".

kusimamiwa na TPPP. Kwa miradi iliyoangukia kwenye Kundi A, vyanzo vingine vya kusaidia miradi husika vitatumika.

Fomu ya Uchunguzi wa Awali wa Mazingira na Jamii iliyokamilika na kupitishwa itaambatanishwa na ripoti ya uchunguzi wa awali (*Scoping report*) na rasimu ya Hadidu za Rejea za TAM vitawasilishwa Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Mamlaka ya Usimamizi wa mradi. TAM mara nyingi itatanguliwa na upembuzi wa awali unaojumuisha utaratibu wa kujiridhisha kwa kina kuhusu masuala ya Mazingira na Jamii, ambapo majibu yatakayopatikana na uchunguzi huo yatasaidia kuandaa Hadidu za Rejea kwa ajili ya TAM. Mamlaka ya Usimamizi wa mradi itafanya mapitio ya ndani ya fomu iliyojazwa kuhusu hali ya Mazingira na Jamii na Hadidu za Rejea na kuwasiliana na Benki ya Dunia kuona kama ina pingamizi ama la kabla ya kuwasilisha kwa NEMC. Hadidu za Rejea za mwisho zitaidhinishwa na NEMC.

ii. **Maandalizi ya TAM na Mpango wa Usimamizi Mazingira na Jamii (MUMJ)**: Kwa miradi ya PPPs ambayo bado haijafanya TAM, Mamlaka za Usimamizi wa mradi zitakuwa na jukumu la kutayarisha TAM ikiwa ni pamoja na MUMJ.[3] Wataalamu waliosajiliwa na NEMC watahusishwa kufanya TAM. Uandaaji wa TAM na MUMJ utafuata mchakato uliowekwa katika ESMF, ambao unazingatia matakwa ya Kanuni za Ukaguzi wa Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii (2005) kama zilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2018 na sera na miongozo ya usalama wa miradi ya Benki ya Dunia. Ripoti za TAM na MUMJ zitafanyiwa mapitio ndani ya Mamlaka za Usimamizi Miradi na kuwasilishwa Benki ya Dunia kuona kama kuna pingamizi au hakuna. Ili miradi ya PPP iweze kuanza kazi, NEMC itawasilisha ripoti za TAM na MUMJ kwa waziri anayehusika na mazingira kwa ajili ya kupata idhini na utoaji wa Cheti cha EIA.

Kwa miradi ya PPP ambayo tayari imeshafanyiwa TAM na kupata Cheti cha EIA mbali na kile cha TPPP, Mamlaka ya Usimamizi wa mradi na Benki ya Dunia zitapitia upya hiyo TAM ili kujiridhisha kama inaendana na sera na miongozo ya usalama wa miradi ya Benki ya Dunia pamoja na matakwa ya ESMF.

iii. **Wajibu wa kutekeleza MUMJ** na kuzingatia sheria na viwango vya kitaifa na sera na miongozo ya usalama wa miradi ya Benki ya Dunia utahamishiwa kwa mbia wa mradi wa PPP kutoka sekta binafsi kwa kupitia mkataba wa PPP. Mabadiliko yoyote au marekebisho ya MUMJ yatakayotokana na mabadiliko yoyote katika muundo wa mradi wa PPP, mabadiliko ya kina ya kiuhandisi au eneo la jengo la biashara au la kutolea huduma yatakayofanywa na mbia kutoka sekta binafsi yatachunguzwa na kufanyiwa tathmini na Mamlaka ya Usimamizi wa mradi na kuwasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupewa idhini. Endapo kutatokea mabadiliko yoyote, basi NEMC itafanya mapitio na idhini kama inavyoelekezwa kwenye kanuni;[4] na

[3] Endapo athari za mradi zinahitaji umakini wa ziada, MUMJ inatakiwa kuhusisha mpango wa usimamizi, mpango shirikishi wa jamii kwa ajili ya kuchukua hatua dhidi ya ukatili wa kijinsia, mpango wa udhibiti wa wanaoomba kazi na mpango wa afya na usalama mahali pa kazi.

[4] Mabadiliko yanaweza yakahitajika kama muundo wa mradi wa PPP utabadilika. Kuandaa muundo wa mradi wa PPP ni zaidi ya kuandaa michoro ya majengo na mazingira yake, kuna mambo mengine ya kuzingatia kama vile matarajio ya huduma na vipengele vya ubora wa huduma na hatua za kupima ufanisi wa mradi katika kutoa huduma na namna ya kugawana hasara.

iv. **Ufuatiliaji na Tathmini na Ukaguzi**: Utekelezaji wa TAM na/au MUMJ utakaguliwa na wakaguzi huru wa ndani watakaoteuliwa na mshirika kutoka sekta binafsi na Mamlaka ya Usimamizi wa mradi na mkaguzi wa nje atateuliwa na NEMC kwa mujibu wa sheria na pia kwa matakwa ya Benki ya Dunia. Utendaji wa mradi wa PPP utafuatiliwa na mshirika wa sekta binafsi pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa mradi.

Washauri wa miradi ya PPP na wataalamu wengine waelekezi wanaotoa ushauri kwa mradi mahususi wa PPP watasaidia tu miradi ya PPP iliyosimamiwa na TPPP. Mathalani hawatakuwa na mamlaka ya kushauri juu ya miradi daraja A ya PPP iliyo chini ya Sera za Usalama wa miradi ya Benki ya Dunia. Miradi ya PPP itafanyiwa uchunguzi wa Mazingira na Jamii kama inavyoelekezwa hapo juu kwenye kipengele cha kutathmini sifa za kukubalika kwa mradi.

## 5. MFUMO WA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO

Kama inavyoagizwa kwenye RPF, kila mradi wa PPP utaanzisha Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko (GRM). GRM itashughulikia malalamiko yote kuhusiana na mradi wa PPP, pamoja na yale yanayohusiana na athari zinazotokana na kuhamisha makazi ya watu na utekelezaji wa RAP/ARAP. GRM imeelezewa kwenye RPF.

## 6. KUJENGA UWEZO

Mafunzo yatatolewa kwa ajili ya vitengo vya PPP, Mamlaka za Usimamizi wa Miradi, na maafisa wanaohusika wa Wizara ya Fedha na Mipango na wa TAMISEMI ili waweze kujengewa uwezo kuhusiana na masuala ya Mazingira na Jamii. Tathmni ya Mahitaji ya Mafunzo (TNA) itafanywa na Mamlaka za Usimamizi wa Miradi ya PPP kwa ufadhili wa TPPP. Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo (TNA) itafanyika kabla ya kuanza TAM na RAP/ARAP. Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo kwa ajili usalama wa miradi itakuwa sehemu ya mpango mpana wa kuzijengea uwezo Mamlaka za Usimamizi wa miradi pamoja na miradi yao ya PPP iliyo chini ya ufadhili wa TPPP wa kujengewa uwezo. Vipindi vya kuwajengea uwezo wa kitaalamu, kupanua uelewa na kuelimisha jamii na kujifunza kwa kutenda vitatolewa.


## 7. UTOAJI WA TAARIFA KWA UMMA NA USHIRIKISHWAJI WA WADAU

Nyaraka za ESMF na RPF pamoja na nyenzo nyingine za usalama wa miradi kama vile ripoti za Tathmini za Athari za Mazingira na Jamii, MUMJ, RAP na ARAP za kila mradi zitapitishwa na Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia na kutolewa kwa umma, na zitakuwa zikipatikana kupitia tovuti (mfano tovuti ya mradi husika wa PPP na tovuti za Mamlaka zinazosimamia miradi) na kutakuwa na tafsiri ya muhtasari wake katika lugha inayozungumzwa kwenye eneo husika kwa kuzingatia utamaduni wa wenyeji. Zitawekwa pia kwenye tovuti za vitengo husika vya PPP na ile ya Benki ya Dunia. Endapo kutakuwa na mabadiliko yoyote katika nyaraka hizi basi utaratibu ule ule wa kuzipitisha utafuatwa.

Wadau walishirikishwa ili kupata maoni yao na hoja zao kuhusiana na ESMF na RPF. Hili lilifanyika kwa awamu mbili. Wadau waliombwa ushauri wao juu ya miradi ya mfano ya PPP inayokuwa inapangwa kuwa chini ya usimamizi wa TPPP wakati wa kuanda pembuzi za awali za miradi 22 ya PPP iliyo chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Awamu kadhaa za mashauriano zilifanyika mfululizo kwa ajili ya kujadili na kushughulikia masuala muhimu yaliyoibuliwa kati ya Juni 2017 na Julai 2018. Ziara za

kutembelea maeneo ya miradi zilifanyika kwa lengo la kuangalia hali za Mazingira na Jamii kwenye Mamlaka za Utekelezaji wa Miradi, taratibu za kitaasisi, uwezo wa kusimamia masuala ya Mazingira na Jamii, na masuala mahususi ya Mazingira na Jamii yanayohusu PPP. Vikao vya mashauriano vilijadili pia kuhusu uhitaji wa kuwa na PPP, muundo wake wa uendeshaji, utayari wa kulipa, muundo wa ujenzi, masuala mahususi ya eneo husika, uhamishaji wa muda wa makazi, na changamoto zinazokabili majengo ya sasa ya kutolea huduma. Taarifa za kina kuhusu wadau walioshirikishwa na maoni yao waliyotoa zimo kwenye Kiambatanisho A. Maoni ya wadau yalitumika wakati wa kufanya mapitio ya ESMF na RPF yaliyofanyika Dodoma kati ya tarehe 5 – 9 Novemba, 2018 na tarehe 20 – 21 Februari, 2019. Wadau walihimizwa kutoa maoni yao kwenye majadiliano ya wazi na wenzao, na warsha hizo ziliendeshwa na maofisa kutoka TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango wanaohusika na usalama wa miradi, na waliomba kupokea maoni kutoka kwa mameneja wa usalama wa miradi wa Mamlaka za Utekelezaji wa Miradi (mfano Mamlaka za Serikali za Mitaa). Ushirikishwaji wa wadau utaendelea kufanyika kipindi chote cha mradi wa PPP unaosimamiwa na TPPP.

***Mchoro 1.1 Mzunguko wa Mradi wa PPP***



RPF sasa inatolewa kwa umma na itapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP), TAMISEMI (kitengo cha PPP) na Kituo cha Habari cha Benki ya Dunia (Info-shop).

Taarifa zaidi zinaweza kupatikana kupitia anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu
Wizara ya Fedha na Mipango,
Mji wa Serikali – Mtumba;
Mtaa wa Hazina,
S. L. P 2802
40468 **DODOMA**
Dodoma
Barua Pepe: ps@mof.go.tz